



# SOLWA:

Mafundi wakifanya kazi ya kuunganisha bomba kuu ku-peleka maji katika manispaa ya Tabora. Mradi unatoa maji katika ziwa Viktoria.



■ Mradi wa Maji wa Miji ya Tabora, Nzega, Igunga na Halmashauri ya Uyui



**MRADI** WA MAJI LAMADI WAFIKIA ASILIMIA 93 uk 6

**RUWASA  
MWAROBAINI  
WA HUDUMA  
YA MAJI  
VIJIJINI** uk 11



# Iguguno na Mgungia: Matumizi ya Mdundiko sasa historia



Mzakiwa wa mkoani Singida akionyesha faida ya mradi wa maji kwa kuanzisha kilimo cha mboga mboga kwa matumizi ya familia yake. Hayo yamekuwa rahisi baada ya uwekezaji wa serikali katika miradi ya maji.

**E**ndapo ulizoea kutumia Mdundiko ukiwa Iguguno au Mgungia, basi jambo hilo hivi sasa ni historia. Wakazi wa Iguguno katika Halmashauri ya Mkalama, na Mgungia katika Halmashauri ya Iramba mkoani Singida hivi sasa wametoka katika safari ya kutegemea matumizi ya Mdundiko na sasa wanapata huduma ya majisafi na salama na yenye kutosheleza kupita pampu zinazotumia nishati ya umeme.

"Mdundiko" ni jina maarufu lililopachikwa kwa pampu za kuvuta maji kwa kusukumwa na mikononi miwili, hata hivyo uwekezaji uliofanywa na Serikali umeleta mabadiliko makubwa kwa huduma ya maji kuwa bora zaidi kwa mamia ya wakazi hawa mkoani Singida. Hivi sasa wananchi katika maeneo haya hawatumii muda mrefu kupata huduma ya maji. Hiyo ndio hali halisi inapofika na kujionea huduma hiyo muhimu baada ya wananchi kuanza kutumia miradi ya maji ya Iguguno na Mgungia.

Ni saa saba mchana, joto lipo juu kadhalika nato jua ni kali nao upepo unavuma kiasi. Ni moja kati ya vitongoji vya eneo la Iguguno mkoani Singida, eneo limezungukwa na vilima vyenye mawe na mashamba. Kwa macho inaonekana jua limewaka hasa, hata majani yamesinyaa lakini mifugo michache inaonekana ikiranda randa huku na kule katika mashamba ambayo ndio kwanza wakulima wamemaliza kuvuna mazao hivyo hakuna uharibifu. Sehemu ya wakazi wa eneo hili wanajishughulisha na kilimo pamoja na ufugaji.

Hali ya hewa na mazingira sio kizuizi kwa kazi nyingine kuendelea kwani Serikali kupitia Mfuko wa Maji wa Taifa imefanikisha miradi ya maji ya Iguguno na Mgungia. Kama inavyoelweka, maji ni maisha na maji ndio kila kitu. Mradi wa maji wa Iguguno una jumla ya vituo 36 vya kuchotea maji kwa wakazi wa eneo hilo pamoja na birika la maji ya mifugo. Mradi wa maji wa Mgungia una vituo vya kuchotea maji 18 na maeneo mawili, ma-

birika, kwa ajili ya maji ya mifugo.

Easter Kitamawe akizungumzia mradi wa maji wa Iguguno anasema kuwa moja ya faida waliyopata katika mradi huo wa maji ni kuacha kutumia visima binafisi ambavyo vilikuwa vina usumbufu, pia kutokua na uhakika wa kupata maji. Anasema kuwa huduma ya maji kwa wenye visima ilikuwa ya bahati nasibu tofauti na hali ilivyo hivi sasa ambapo maji yapo ya kutosha.

Maria Kitawa, anayeishi Iguguno anasema miradi ya maji imeleta mwamko tofauti kutokana na hali ilivyokuwa awali ambapo wananchi walipotewa muda mwingi kutafuta maji. Anasema hivi sasa watu wanahitaji kuunganishwa maji katika makazi yao.

Kitawa anasema kuwa jamii imeona umuhimu na manufaa ya maji kuwa karibu zaidi kwa kurahisisha mambo mengi na kuokoa muda uliokuwa ukitumika kutafuta huduma hiyo katika maeneo ambayo hayakuwa salama na kutiliwa shaka ubora wake. "Maji yalichukuliwa katika makorongo bila kujali wanyama wamekunywa au yamechafuliwa" Kitawa anasema.

Miradi ya maji iliyofanikishwa na serikali imepunguza gharama zilizokuwa zikitumika kununua maji au bei za juu zilizokuwa zikiwekwa na wafanyabiashara wa maji. Kurwa Shamkulusi ni mmoja kati ya wafanyabiashara ya maji ambaye anaona mambo yamebadilika kufuatia ujio wa miradi ya maji, amekua akifanya kazi hiyo toka mwaka 2001 akiwa Iguguno.

"Kabla ya mradi niliweza kujiingiza kipato cha shilingi elfu 12 hadi elfu 15 kwa siku kwa kuza madumu ya lita 20 yapatayo 100 kwa siku" Shamkulusi anasema na kungeza hivi sasa mambo yamebadilika na kiwango anachopata hakizidi shilingi elfu tano, hali hiyo inamfanya kufikiria jambo jingine zaidi la kuingiza kipato kwa sababu huduma ya maji sasa imekuwa karibu na makazi ya waliokuwa wateja wake, hivyo hawa-

hitaji huduma yake kama mwanzo.

Patience Chale, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Iguguno anasema kuwa kwa muda aliofanya kazi baada ya mradi wa maji hakuna matatizo yanayotokana na magonjwa ya mlipuko kwa kusababishwa na maji. Anasema mradi wa maji ni mafanikio makubwa, na lengo sasa ni kuifikisha katika maeneo mengine ambapo nao wanahitaji wa huduma ya maji kuwa karibu zaidi.

Mhandisi Omari Matembo anasema kuwa mradi wa Iguguno hivi sasa una miaka mitano na umekua wa kisasa zaidi. Anasema zamani zilitumika pampu zilizotumia nguvu ya mikononi hali ambayo ni tofauti na hivi sasa ambapo nishati ya umeme inatumika.

Matembo anasema mkakati uliopo hivi sasa ni kutafiti vyanzo vya maji vingi zaidi na kungeza ubora wa huduma ya maji kwa wananchi.

Bi. Maria Kitundu, mkazi na mwenyeji wa Iguguno anasema kabla ya mradi kipindi cha kiangazi ndicho kilikuwa na changamoto zaidi. Maji katika mabonde yalikuwa yanakauka, hivyo kuchimba ili kuyapata, pamoja na hayo hayakuwa salama sana. Anaongeza kuwa magonjwa nayo yaliwaandama kila uchao kutokana na maji kutokua bora.

Anasema uwepo wa huduma ya maji kumemwezesha kufuga kuku kiasi, pia kupunguza gharama aliyokuwa akiitumia kutafuta maji. "Hivi sasa natumia shilingi elfu tano kwa mwezi mzima katika maji" Bi. Kitundu anasema na kusesitiza imekuwa ahueni kubwa kwani kiasi hicho kilikuwa hakitoshi kwa siku nne kwa matumizi ya maji nyumbani kabla ya mradi wa maji. Bi. Kitundu anasema kuwa gharama za matumizi ya familia yake katika maji zimepungua na fedha anaweza kuitumia katika kazi nyingine za maendeleo, ikiwamo kuanzisha biashara ndogo ndogo za mboga.

Hamsi Jama ambaye ni mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumiaji Maji itwayo WASOWA wa mradi wa maji wa Mgungia katika Wilaya ya Iramba, kata ya Kasehya anasema mabadiliko yaliyoletwa na mradi huo ni kubwa. Moja ya faida anasema ni mifugo kuwa bora zaidi ikiwamo ng'ombe kutoa maziwa mengi zaidi ya ilivyokuwa awali.

Mwenyekiti huyo anasema mifugo haipotelewi mbali ili kunywa maji kwa sababu huduma hiyo imeletwa katika makazi yao. WASOWA inasimama kwa maana ya Asante, WA ikiwakilisha Wabeja-kwa Wasukuma, SO ikimaanisha Songeta - kwa Kinyiramba na Wa ikimaanisha Wajijya kwa Kinyaturu. Imekua hivyo kwa sababu ni eneo lenye mchanganyiko wa makabila na mahitaji ya maji kwa kazi tofauti tofauti za maendeleo. Nia hasa ni kusema asante kwa kazi iliyofanyika ya kufikisha maji kwa wananchi hao, ambao wameyatumia kuongeza thamani ya shughuli zao za kila siku.

Kwa Ollian Stephen, ambaye ni Mtendaji wa Kijiji cha Mgungia anasema kuwa mradi huo wa maji ni mkombozi kwao na watahakikisha

unakua endelevu. Anasema maji ni ya uhakika na wanavyo vifaa wanavyoweza kuvitumia katika kutatua matatizo madogo madogo mara yanapojitokeza katika mradi. Ufundi huo umewezeshwa na wataalam wa maji wa halmashauri ya Mkalama. Endapo tatizo kubwa linatokea wataalam wa maji yenyewe wanahusika moja kwa moja kwa kupewa taarifa, anasema Stephen.

Bi. Zaituni Jumanne ambaye ni mkazi wa kijiji cha Mgungia, kwake ni siku nyingine ya kujitafutia riziki na kusukuma gurudumu la maendeleo mbele. Bi. Jumanne ametoka sokoni kujitafutia mahitaji ya nyumbani, hali ambayo kwa miaka iliyopita anasema ingekuwa tofauti, angekuwa hatoki sokoni bali angekuwa na ndoo ya maji kichwani au katika baiskeli ili kukidhi mahitaji ya familia yake.

Hivi sasa Bi. Jumanne anapata maji katika mradi wa maji wa Mgungia na haitaji kwenda umbali mrefu kubeba maji tena. Mradi wa maji umemwezesha kuongeza idadi ya mifugo ambayo pia inamwingizia kipato. Hivi sasa anamiliki ng'ombe watano. Anasema kuwa kabla ya mradi ingekua ngumu kuwa na kiasi hicho cha mifugo nyumbani, kwani maji ya kuhudumia familia bado ilimchukua muda mrefu kuyatafuta, kwa wakati huo pipa la maji la ndoo 12 lilinuliwa kwa shilingi 3,000 lakini sasa hali imebadilika kwani inatumika shilingi 600 kwa kiasi hicho hicho.

Serikali inaendelea kuwekeza katika miradi ya maji kwa kutumia gharama kubwa, na miradi hii ni ya wananchi. Hadi ifikapo mwaka 2020 lengo ni kufikisha huduma ya maji kwa asilimia 85 maeneo ya vijijini. Miradi hii ni fursa kwa wananchi kuitumia kuongeza thamani ya bidhaa wanazozalisha, na kuwajibika kwa kutunza vyanzo vya maji ili viwe endelevu. Idadi ya watu inaongezeka lakini rasilimali maji haiongezeki. Pamoja na hilo, kila mwananchi anatakiwa kulinda na kuteriza miradi ya maji kila wakati.

Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Namba 5 ya mwaka 2019, iliyoanza kutumika mwezi Julai 2019 imeweka bayana adhabu mbalimbali kwa yeyote atakayeharibu au kuchezea miundombinu mbinu ya majisafi na majitaka. Moja ya adhabu ni kulipa faini ya shilingi laki tano hadi milioni tano au kifungo cha kuanzia miezi 12 hadi miaka mitano.

Maji ni rasilimali muhimu kwa maisha ya viumbe hai, mimea, na mazingira. Maji ni bidhaa muhimu kwa maendeleo ya nchi kwani ndio yanayotumika katika uzalishaji wa nishati inayotumika kuendesha viwanda vikubwa na vidogo, pia utalii na kilimo. Hivyo, ni nyenzo ya kutokomeza umasikini na kukuza uchumi kwa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Tafti zinaonyesha kuwa hadi mwishoni mwa miaka ya 60 kiwango cha maji kwa kila mtu hapa nchini kilikuwa wastani wa mita za ujazo zaidi ya elfu 10, lakini hadi mwaka 2018 kiwango hicho kilishuka hadi kufikia mita za ujazo 2,332.



# MRADI WA MAJI WA MUGANGO - KIABAKARI- BUTIAMA:

## Kukamilika ndani ya miezi 24

**M**kataba wa kuanza utekelezaji wa mradi wa maji wa Mugango - Kiabakari - Butiama umesainiwa Agosti 15, 2019 katika viwanja vya shule ya msingi Nyamisisiye (Kiabakari) na kushuhudiwa na viongozi pamoja na baadhi ya wakazi wa mkoa wa Mara.

Mkataba huo umesainiwa baina ya serikali na kampuni za Metito (Overseas) kutoka Misri na kampuni ya Jandu Plambers ya nchini.

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo akiongea katika hafla hiyo amesema serikali imeamua kutumia ziwa Viktoria kama chanzo cha maji kwa miradi ya maji itakayotekelezwa maeneo ya kanda ya ziwa. Aidha, amesisitiza utaalam utazingatiwa ili kuepuka matatizo kwa watumiaji wengine wanaotegemea ziwa hilo.

Prof. Kitila amesema hadi itakapofika mwanzoni mwa mwaka kesho 2020 serikali itakua imetumia kiasi cha shilingi trilioni 1.3 kwa uwekezaji wa miradi ya maji ya kuhudumia wananchi katika maeneo mbalimbali ya kanda ya ziwa.

Ameongeza kuwa miradi hiyo inayotekelezwa ni ya wananchi hivyo kila mmoja kwa nafasi yake afuatilie maendeleo yake, na endapo kuna tatizo taarifa itolewa bila kusita ili hatua zichukuliwe mara moja.

Prof. Kitila ameongeza kuwa uwekezaji wa serikali katika miradi ya maji umongezwa hali ya upatikanaji maji nchini hadi kufikia asilimia 71, ambapo takwimu zinaonyesha toka awamu ya tano iingie madarakani kwa vijijini hali ya upatikanaji maji imepanda kutoka asilimia 46 mwaka 2015 hadi asilimia 64 mwaka 2019, na mijini kwa kipindi hicho imetoka asilimia 74 hadi asilimia 84.

Mradi wa maji wa Mugango - Kiabakari - Butiama unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24 kuanzia tarehe ya kusainiwa mkataba na utaongeza hali ya upatikanaji maji katika maeneo husika kutoka asilimia 67 ya sasa hadi kufikia asilimia 100. Mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ambao ni Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (SFD).



Mkuu wa Mkoa wa Mara Mhe. Adam Malima akiongea na wananchi wakati wa hafla ya utiaji saini wa mradi wa maji wa Mugango - Kiabakari - Butiama



Katibu Mkuu Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo (kulia) akikabidhi mkataba wa kuanza ujenzi wa mradi wa maji wa Mugango - Kiabakari - Butiama kwa mwakilishi wa kampuni ya Metito katika hafla iliyofanyika hivi karibuni mkoani Mara.



atibu Mkuu Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo (kulia) akisaini mkataba wa mradi wa Mugango - Kiabakari - Butiama, pamoja na mwakilishi kutoka kampuni ya Metito.

### Ndugu wasomaji,

Karibuni katika Jarida Tando linalohusu masuala ya sekta ya maji.


Lengo ni kuhakikisha matukio na maendelea mbalimbali yanayofanyika katika sekta ya maji yanaandikwa na kuwafikia wadau wengi.

Hivyo, endapo kuna utafiti uliofanyika kuhusu sekta ya maji, mradi uliotekelezwa au maboresho ya mradi ili wananchi wapate huduma bora tupe taarifa, usisite kuwasiliana nasi.

Jarida linatoka mara moja katika miezi mitatu.

Mawasiliano:  
gcu.staff@maji.go.tz  
www.maji.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MAJI

**DIRA:**  
Kuwa na huduma ya majisafi na salama iliyotekelezwa, nafuu na ya kutosha kwa wananchi wote.

**DHAMIRA:**  
Kuhakikisha rasilimali za maji zinasimamiwa, zinaendelezwa na zinatumika kwa njia endelevu na shirikishi ili kukidhi mahitaji mbalimbali kwa kuweka mfumo madhubuti wa kitaasisi wa kusimamia rasilimali za maji; na kuboresha miundombinu ya usambazaji majisafi na uondoaji majitaka.

**MAADILI YETU:**  
 ■ Ushirikiano ■ Uadilifu ■ Uwajibikaji ■ Ubora ■ Ubinifu

**MAJUKUMU YA WIZARA**

- Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji;
- Kutayarisha na kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Maji;
- Kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji; Sekta ya Maji;
- Kutoa miongozo ya usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali za maji;
- Kutoa miongozo ya utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini;
- Kutoa mafunzo kwa wataalam wa Sekta ya Maji katika ngazi na kada mbalimbali za utekelezaji;
- Kuendeleza tafti kuhusu teknolojia zinazotumika katika kutoa huduma ya maji;
- Kuratibu majukumu na kutekeleza ushauri wa Bodi ya Taifa ya Maji.
- Kuhakiki ubora na usalama wa maji katika vyanzo vya maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi na mazingira;
- Kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama na ya kutosha katika maeneo yao na;
- Kuhakikisha rasilimali za maji zilizo zinalindwa, zinahifadhiwa na kuendelezwa katika namna ambayo zitakuwa endelevu;

Mawasiliano yetu —  
 📍 Mji wa Serikali, Mtaa wa Maji, S. L. P. 456, DODOMA,  
 ☎ +255 26 2322602 ✉ ps@maji.go.tz 🌐 www.maji.go.tz

Mitandao ya Kijamii  
 📺 WizarayamajiTanzania 📱 MajiTanzania 📧 WizarayamajiTz 📺 WizarayamajiTanzaniaMajLmoot





Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji Eng. Emmanuel N.M. Kalobelo (mwenye kofia) akikagua mradi wa maji wa Nguruka, wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma. Eng. Kalobelo katika ukaguzi huo amemtaka mkandarasi kukamilisha ujenzi wa kazi zilizobaki ndani ya mwezi Septemba 2019 ili wananchi wanapate huduma ya maji kila wakati.







Katibu Mkuu Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo akiongea na Maafisa Habari na Mawasiliano kutoka taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji , katika kikao kazi kilichofanyika Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro. Prof. Mkumbo katika kikao hicho aliwataka washiriki kuwashirikisha wananchi kwa taarifa mbalimbali kuhusu maendeleo ya sekta ya maji nchini.



Prof. Mkumbo katika picha ya pamoja na washiriki.



Miundombinu ya mradi wa Lamadi ikiwa katika hatua za mwisho kabisa za ujenzi kabla wananchi hawajaanza kupata huduma ya majisafi na salama.

Na Mohamed Saif - Mwanza

**N**aibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Emmanuel N.M Kalobelo amesema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi wa maji wa Lamadi katika Wilaya ya Busega Mkoani Simiyu ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 93.

Mhandisi Kalobelo aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa ziara yake kwenye mradi na washirika wa maendeleo wanaowezeshwa utekelezaji wa miradi ya maji kupitia Programu ya Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ijulikanayo kama LV WATSAN ambao ni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD).

Alisema amefarijika kushuhudia hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa mradi na aliongeza kuwa hadi robo ya kwanza ya mwaka 2019/2020 ikiisha kazi ya ujenzi wa mradi itaku imekamilika. Kazi iliyosalika hadi wakati wa ukahuzi ilikuwa ufungaji wa pampu.

Akizungumzia hali ya mji wa Lamadi kabla ya ujenzi wa mradi, Naibu Katibu Mkuu alisema mji huo kwa muda mrefu ulikuwa na ukame na kwamba mradi wa maji ni mkombozi kwa wananchi wa maeneo hayo na unadhihirisha matumizi sahihi ya Ziwa Viktoria.

Aliwataka wananchi wanaozunguka Ziwa Viktoria kuhakikisha wanatunza mazingira hasa ikizingatiwa kwamba manufaa wanayoyapata ni makubwa kwao na kwa vizazi vijavyo. "Tuepuke uchafuzi wa ziwa, tuendeleo kutunza mazingira yetu kwani maji haya tunayatumia kwa shughuli mbalimbali," alisema.

Kwa upande wake Mratibu mradi kutoka EIB, Raoul Pedrazzani alisema miradi inayotekelezwa chini ya Programu ya LV WATSAN imeonyesha mafanikio makubwa na alipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) ambayo inajukumu la kusimamia miradi hiyo kwa niaba ya Wizara ya Maji kwa usimamizi mahiri wa utekelezaji wake.

Pedrazzani alisema EIB inayo nia ya dhati ya kupanua ushirikiano na serikali ya Tanzania katika siku zijazo kwani imeridhishwa na namna ambavyo Serikali inatekeleza miradi maeneo mbalimbali kote nchini.

Naye Afsa Miradi kutoka AFD, Mhandisi Clement Kivegalo (sasa Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA) akizungumza kwa niaba ya ujumbe alioambatana nao, alisema wameridhishwa na hatua ya utekelezaji wa mradi na kwamba AFD itaongeza udhamini kadri itakavyohitajika kufanya hivyo.

"Tunafurahi kwamba ipo miradi mingine inaendelea kutekelezwa kupitia MWAUWASA, tunatarajia kuongeza udhamini wa miradi kwa lengo la kuongezea Mamlaka uwezo wa kuzalisha maji na upanuzi wa mtandao wa usafirashaji maji kwenda maeneo mengine ambayo hayana maji," alisema Kivegalo.

Aliongeza kuwa AFD inajihusisha zaidi na masuala ya maji na alibainisha kwamba ipo miradi mingine am-

## MRADI WA MAJI LAMADI WAFIKIA ASILIMIA 93

bayo inategemea kufadhiliwa katika Mikoa ya Shinyanga na Dar es Salaam.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Busega, Tano Mwera, alisema mradi unatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa kwenye wilaya na hususan katika mji wa Lamadi.

Alitoa wito kwa wawekezaji kujitokeza kwa wingi kuwekeza kwenye wilaya hiyo kwani tayari maji ya uhakika yamepatikana na kwamba miundombinu mingine pia ipo ikiwemo umeme wa uhakika na barabara.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga kuhusu mradi wa Lamadi alisema unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia mia moja kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka EIB na AFD kwa gharama ya Shilingi Bilioni 12.83.

Mhandisi Sanga alisema mradi utazalisha lita Milioni 3.3 za maji kwa siku ambayo ni mara mbili ya mahitaji ya

sasa ya wananchi wa Lamadi na maeneo jirani hasa ikizingatiwa kwamba mradi umebuniwa kuhudumia wananchi zaidi ya 60,000.

Aliongeza kuwa hatua ya kwanza ya maunganisho kwa wananchi; mradi utaunganisha kaya zipatazo 5000 na aliwataka wananchi kuchangamkia mradi ili kujiletea maendeleo.

Mradi wa maji wa Lamadi unatekelezwa na Mkandarasi ambaye ni kampuni ya CCECC kutoka China na ni sehemu ya Programu ya Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (LV WATSAN) unatekelezwa vilevile katika Jiji la Mwanza, Miji ya Musoma, Bukoba, Miji midogo ya Magu na Misungwi kwa gharama ya shilingi Bilioni 276.



06

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Emmanuel N.M Kalobelo (wa pili kutoka kushoto) akikagua mradi wa maji wa Lamadi. Anayefuata ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) Mhandisi Anthony Sanga.



# Mradi wa majitaka Mwanza unavyovutia wageni Duniani

Na Mohamed Saif -Mwanza

**S**erikali imeweka kipaumbele kuhakikisha huduma kwa wananchi ya majisafi na salama katika Jiji la Mwanza inakuwa ya uhakika.

Kufanikisha hilo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA), inaendelea na juhudi katika kuhakikisha wananchi wanapata majisafi, salama na yenye kutosheleza.

Juhudi mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na MWAUWASA kuhakikisha wananchi wote wanafikiwa na huduma hiyo kama ambavyo serikali ya awamu ya tano ilivyopanga.

Pamoja na ujenzi wa miundombinu ya majisafi na salama, MWAUWASA inatekeleza ujenzi wa mradi wa mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka kwenye maeneo ya milimani unaofahamika kitaalamu kama 'Simplified Sewerage System'. Miongozi mwa wakazi wa jiji la Mwanza makazi yao yapo katika maeneo ya milima.

Wadau wa sekta ya maji, kutoka mataifa mbalimbali wameshafika hapa nchini kujionea na kujifunza kuhusu mradi huo wa majitaka milimani. Miongoni mwao walitoka katika Asasi za Kiraia (AZAKI) kutoka nchi za Brazili, Afrika ya Kusini, Kenya na Uganda.

Nchi hizo zimevutiwa na ubunifu uliotumika katika ujenzi wa mradi huo wa uondoshaji majitaka kwenye maeneo ya milimani. Katika mahojiano maalumu na Jari-da hili, Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali linaloji-shughulisha na masuala ya kijamii nchini (CCI), Dk. Tim Ndezi, anazungumza mambo mbalimbali kuhusu ujenzi huo.

Dk. Ndezi ndie alikuwa mwenyeji wa ugeni huo kwa hapa nchini, anasema mradi huo umeendelea kuwa kuvituo kikubwa kwa mataifa mbalimbali duniani.

Anasema taasisi zinazojishughulisha na masuala ya usafi wa mazingira kutoka nchi mbalimbali baada ya kupata sifa za mradi huo zimevutiwa na kufanya ziara ili kujifunza zaidi ubunifu uliotumika katika utekelezaji waki ili pia kutumia katika nchi wanazotoka.

"Wageni hawa wamekuja kujifunza namna ambavyo

mradi huu umejengwa ili nao wakaandae mradi wa namna hii kwenye nchi zao," Dk. Ndezi anasema.

Mradi huo umeendelea kutembelewa na wageni kutoka mataifa mbalimbali kwa lengo la kujifunza namna ulivyotekelezwa na namna ambavyo unaendeshwa.

Kwa mujibu wa Dk. Ndezi, ugeni huo ulilenga kuzunguruma na wanufaika wa mradi huo ili kufahamu wajibu wao na namna ambavyo waliupokea na njia wanazotumia kuutunza.

Wageni wa mwanzo kutembelea mradi walitoka nchini Kenya ambao lengo rasmi lilikuwa kujifunza namna bora ya kutekeleza mradi wa majitaka hususan kwa maeneo yasiyo rasmi.

Ugeni huo wa awali kutoka nchini Kenya ulieleza namna ulivyovutiwa na ubunifu mkubwa uliotumika katika ujenzi wa mradi wa majitaka kwenye maeneo ya milimani.

Wageni hao kutoka Kenya walihadi kurejea tena nchini na wataalamu wa mamlaka zinazohusika ili kujenga miradi ya namna hiyo nchini kwao.

## UGANDA WAZUNGUMZA

Mmoja ya wageni kutoka Uganda, Mundamba Omar, anasema nchi hiyo inayo changamoto ya wananchi wake hususan wa kipato cha chini kukosa mfumo bora na rasmi wa uondoaji wa majitaka.

Anasema ziara hiyo walioyifanya Jijini Mwanza ime-wapatia uzoefu na ujuzi wa namna ya kujenga na kusimamia mradi mzuri wa majitaka.

"Tunaipongeza MWAUWASA, kazi iliyofanyika hapa ni ya kipekee, hatuna budi nasi kuiga," Omar anasema. Mradi huo wa majitaka milimani ni miongoni mwa miradi miwili bora zaidi kutekelezwa Barani Afrika, chini ya ufadhili wa African Infrastructure Trust Fund (EU-AITF).

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga, ujenzi wa mradi huu ulianza mwaka 2016 na umenufaisha kaya zipatazo 415. Mhandisi Sanga anasema mradi ulijengwa kwa majaribu katika maeneo matatu ambayo ni Kilimahewa, Mabatini na Igogo.

Katika maeneo hayo, Mhandisi Sanga anasema mwi-tikio ulikua mzuri na alitolea mfano kwa Kilimahewa ambapo MWAUWASA ilipanga kuunganisha kaya 68.

Hata hivyo, kutokana na mwikikio kuwa mkubwa, kaya 117 ziliunganishwa na kwa upande wa Mabatini mpango ulikua ni kuunganisha kaya 88, ambapo zaidi ya kaya 178 ziliunganishwa na kufikia jumla ya kaya 415 kwenye maeneo yote matatu.

Mhandisi Sanga anabainisha kuwa awamu ya pili ya ujenzi wa mradi huo, itahusisha maeneo mengi zidi ambayo ni Kabuhoro, Ibungilo, Kawekamo na Isamilo.

"Maeneo ambayo tulianza nayo kwenye awamu ya kwanza nayo hatujamaliza, kwa hiyo haya ni maeneo mapya, lakini pia tutarudi kwenye hayo maeneo ya awali tukaunganishe kaya zilizosalia," Mhandisi Sanga anafanua. Akielezea sababu za mradi huo kuitwa mfumo rahisi, Mhandisi Sanga anasema mradi ulipunguza baadhi ya vigezo kwenye miongozo ya usanifu miradi kutoka Wizaru ya Maji.

"Ukivifuata vigezo vyote kama vilivyo kwenye miongozo inakuwa ngumu kutekeleza mradi kwenye maeneo ya namna hiyo," Mhandisi Sanga anafanua.

Anaongeza changamoto iliyopo kwenye Jiji la Mwanza ni kwamba zaidi ya asilimia 70 ya maeneo hususan ya milimani hayajapimwa, hivyo kusababisha ujenzi wa miradi kuwa mgumu.

Anabainisha kwa Tanzania, Jiji la Mwanza ni la kwanza kutekeleza miradi ya namna hiyo na kwa Dunia, miradi ya namna hiyo inapatikana nchini Brazili.

Mhandisi Sanga anasema lengo mahsusi la mradi huo ni kuondosha majitaka kwa njia rahisi kutoka kwenye maeneo ya milimani ili kuwapeusha wakazi na maradhi yanayoweza kutoka kutokana na mfumo usio rasmi wa uondoshaji wake na kusisitiza kuwa lazima kuhakikisha majitaka yanatolewa na yanatibiwa kwa kuwa yanaweza kuwa hatari kwasababu mara nyingine hua ni chanzo kikuu cha maradhi. Anasema awali uondoshaji wa majitaka kwenye maeneo ya milimani Jijini Mwanza ulionekana kuwa mgumu na kutowezekana.

"Ni lazima tuwe na majawabu kwenye maeneo ambayo hapo zamani ilionekana hayawezekani kabisa," Mhandisi Sanga anasisitiza.

Diwani wa Kata ya Mbugani, Athumani Jama, anasema kabla ya mradi huo hali ilikuwa ni chafu hasa ikizingatwa hali halisi ya kijiografia ya maeneo ya milimani. Anaongeza kuwa vyo vya mashimo vilitumika na vilikuwa vifupi, na wakati wa mvua hali ilikuwa mbaya, maji yalikuwa yanatiririka ovyo na magonjwa ya mlipuko yalikuwa ya kufikia tu.



Ugeni kutoka Brazili, Afrika Kusini, Kenya na Uganda ukiwa katika moja ya eneo lenye mradi wa majitaka milimani, simplified sewerage, Jijini Mwanza.

# HUDUMAYA MAJI SONGWE YAIMARISHWA



Banio jipya la maji la Vwawa

**S**erikali inatekeleza miradi ya majisafi na usafi wa mazingira mkoani Songwe ili kuboresha na kuimarisha hali ya upatikanaji maji kwa wananchi katika mkoa huo. Miradi hiyo inatekelezwa katika miji ya Vwawa na Mlowo.

Miradi hii itaongeza hali ya upatikanaji maji kwenye miji ya Vwawa na Mlowo kutoka asilimia 35 ya sasa hadi kufikia asilimia 56.

zinaonyesha kuwa kwa mwaka 2019/20, miji ya Vwawa na Mlowo inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi 117,198 na wastani wa mahitaji ya maji ni lita milioni 9.558 kwa siku.

Miradi hii itanufaisha wananchi kwa kutatua changamoto za utoaji huduma ya maji kwenye miji ya Vwawa na Mlowo.

08

Changamoto hizo ni pamoja na; maji yanayozalishwa kutotosheleza ambapo maji yanayozalishwa kwa sasa yanafika asilimia 44.5 ya mahitaji, na kuondosha mgao wa maji. Hata hivyo, elimu inatolewa ili kumaliza changamoto kwa shughuli za kibinadamu kufanyika katika vyanzo vya maji.

Vyanzo vya maji vina-vyotumika ni vijito vya Mgombezi, Nalabana Haloli, Mto Mantengu, Mto Mlowo, Chechemi ya Lutumbi, Chemchemi ya Mbozi club na kisima kirefu cha Ichenjezya.

Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Vwawa – Mlowo ilianzishwa mwaka 2016 na inatoa huduma ya maji kwenye miji ya Mlowo na Vwawa ambayo ni makao makuu ya Mkoa wa Songwe.



Mtambo mpya wa kusafisha maji wa Vwawa





Waziri wa Maji, Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb) – mwenye miwani, akiwa katika picha ya pamoja na wakazi wa kijiji cha Kazingumu, mkoani Manyara akiwa ziara ya kikazi kukagua miradi ya maji.



Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akizungumza na wakazi wa Kijiji cha King'ori, wilayani Arumeru, Mkoani wa Arusha kuhusu huduma za maji na hatua zinazochukuliwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya maji.



Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo akiongea wakati wa hafla ya kuweka saini mkataba wa kazi ya ujenzi wa mradi wa maji wa Mugango - Kiabakari - Butiama



Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiwa katika kisima cha maji cha Mbuguni kitakachotumika kama moja ya chanzo cha Mradi wa Maji wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya Arumeru.



# MAMLAKA YA MAJI MUSOMA:

## Yajipanga kufikisha huduma ya maji kwa asilimia 100

### # Yaanza kutekeleza agizo la JPM

**M**amlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) imeanza ujenzi wa Tangi la maji la Bharima ikiwa ni kutekeleza agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli alilolitoa tarehe 05 Septemba 2018 wakati akizindua mradi mkubwa wa majisafi wa Bukanga katika Manispaa ya Musoma.

Mradi huu utahusisha usimikaji wa pampu ya kusukuma maji pamoja na mtandao wake. Mradi huu utajengwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza utahusisha ujenzi wa tangi la Bharima lenye ukubwa wa mita za ujazo 3,000; pampu ya kusukuma maji, bomba la kupeleka maji kwenye tangi la urefu wa kilomita 1.7 (pumping main 450mm pipe), bomba la usambazaji (450 mm size gravity pipe main) kilomita 6.8 na mabomba madogo madogo ya usambazaji maji katika Manispaa ya Musoma yenye urefu wa kilomita 44.3.

Mradi huu kwa awamu ya kwanza unatekelezwa kwa miezi 18 na mkandarasi kampuni ya Jandru Plumbers Ltd. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 9.4. Pamoja na hilo, Mamlaka pia imeanza utekelezaji wa ujenzi wa mfumo wa kutibu majitaka na unatekelezwa na mkandarasi kampuni ya JR International kwa thamani ya shilingi Bilioni 26 na utakamilika katika kipindi cha miezi 18 kuanzia mwezi Oktoba, 2018. Mradi huu unatekelezwa na serikali ya Tanzania kwa ushirikiano na washirikia wa maendeleo ambao ni Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na Banki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) kwa mkopo nafuu.

Mradi huu miongoni mwa mengine, utahusu mabwawa makubwa ya kutibu majitaka, ulazaji wa mabomba kwa ki-



**Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) Mhandisi Robert Lupoja.**

lomita 50, ujenzi wa vituo vinne (4) ya kusukuma majitaka, uunganishaji wa wateja wapatao 1,200 katika mfumo wa majitaka na ujenzi wa jengo la ofisi ya mamlaka. Aidha, kutakua na ujenzi katika baadhi ya maeneo ya huduma kwa jamii kama shule.

MUWASA tayari ina magari mawili kwa ajili ya huduma ya majitaka na majisafi. Gari moja litatumika kwa uondoaji wa majitaka kwa wakazi wa Manispaa ya Musoma kwa gharama nafuu na pia gari lingine litatumika kupeleka huduma ya majisafi katika maeneo ya pembezozi yasiyofikiwa na mtandao wa maji.

Mkakati wa kuimarisha huduma kwa wateja unaendelea ambapo mamlaka ipo katika mpango wa kununua Dira za maji 6,300 za kawaida na nyingine 160 za malipo kabla. Wateja wote wasio na Dira na wenye Dira Mbovu watafungiwa Dira hizo. Kazi hii itafanyika Septemba 2019.

Katika kurahisha malipo kutoka kwa wateja, mabadiliko makubwa

yamefanyika ambapo hivi sasa mamlaka imejiunga na mfumo wa kieltroniki wa kukusanya mapata (GePG) na wateja wanaweza kulipa Ankara zao kupitia mitandao yote ya simu, Benki zote na mawakata wa benki.

MUWASA inazalisha maji yanayotumiwa na wateja katika kituo kipya cha kutibu maji (Conventional Water Treatment Plant) kilichopo Bukanga ambacho kilizinduliwa rasmi tarehe 5 Septemba, 2018 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli. Kituo hiki kinazalisha maji kwa wastani wa mita za ujazo 36,000 kwa siku ambapo kwa sasa tunazalisha mita za ujazo kati ya 18,000 na 21,000 kuendana na mahitaji ya maji kwa siku.

Aidha, kipo kituo kingine kidogo cha uzalishaji maji cha Bweri ambacho maji yake hutoa huduma kwa baadhi ya wakazi wa maeneo ya Bweri. Hata hivyo, kituo hiki kitafungwa na baada ya muda mfupi wateja wote watapata huduma ya maji kutoka kwenye chanzo kipya cha Bukanga.

Wateja wa MUWASA hivi sasa wameanzishwa eneo maalum, kitenge cha huduma kwa wateja ambacho kitawahudumia wateja kwa kupokea kero mbalimbali na changamoto wanzokumbana nazo katika huduma na kupokea taarifa za hitilafu kuhusu miundombinu ya maji. Namba itakayotumika katika kitenge hiki ni 0800110108, na itapatikana bila malipo. Huduma bora kwa wateja inafanyika sanjari na kazi ya kuingeza mtandao wa maji imefanyika kwa urefu wa kilomita 21 kupitia makusanyo ya mamlaka. Aidha, nguvu kazi ya wananchi imetumika katika kufanikisha kazi hii.

Huduma ya maji itaboreshwa zaidi kwa utekelezaji wa miradi ifuatayo katika Manispaa ya Musoma.

Eneo la Bweri linalopata maji yasiyotibiwa kwa hatua zote, kazi ya uunganishaji wa bomba la mm 200 kwa urefu wa kilomita 1.2 kutoka njia panda Songe mpaka Bweri. Kazi hii itafanyika

mwishoni mwa Septemba 2019. Kazi hii itafanyika sambamba na ulazaji wa bomba la mm 200 kwa urefu wa kilomita 2.5 kutoka eneo la Sanane Sandeep hadi Rwamlimi.

Katika mpango wa muda wa kati Mamlaka imejipanga kuboresha upatikanaji wa maji katika eneo lake kwa asilimia mia katika ya Manispaa ya Musoma na vilevile maeneo yaliyo nje ya Manispaa ya Musoma, yaani katika wilaya ya Butiama pamoja na Musoma Vijijini.

Aidha, mamlaka inajipanga kulaza mabomba ya mtaa yenye jumla ya km 52.6 katika maeneo ya Kwangwa, Songambele na Rwamlimi, Nyabisare, Bweri ya Bukoba na maeneo yaliyo juu na Nyabange eneo lililopo Wilaya ya Butiama. Kazi hii itahusisha usimikaji wa pumpu ndogo Kigera na Ujenzi wa tenki dogo Kwangwa.

Mipango hii ya mamlaka itakamilika mwishoni mwa mwaka 2020 kwa kufikia lengo la kuingeza upatikanaji wa huduma ya maji kufikia asilimia 95 katika miji mikuu ya mikoa. Hivi sasa asilimia ya upatikanaji maji katika mji wa Musoma ni asilimia 82 na mpango ni kufikia asilimia 100. Pamoja na hilo, mamlaka inaendelea kusimamia miradi ya maji iliyopo katika miji midogo ya Bunda, Sirari, Rorya, Mugumu, Tarime na Shirati.

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) ilianzishwa kwa Sheria ya Maji Na. 8 ya Mwaka 1998, na kufanywa marekebesho kwa Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019.

MUWASA inatoa huduma ya maji katika eneo la Manispaa ya Musoma lenye ukubwa wa kilomita za mraba 63 na wakazi wapatao 171,009 (sense ya makazi na watu ya mwaka 2012). Aidha, inatoa huduma katika eneo la Nyabange, Halmashauri ya Wilaya ya Butiama. Hadi mwezi Julai 2019 MUWASA ilikua na jumla ya wateja wateja 15213.



**Naibu Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akizindua Magari yatakayotoa huduma ya Majitaka na Maji Safi wakati wa ziara ya kikazi katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) hivi karibuni.**



**Naibu Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), aliyebeba tofali, akishiriki kazi ya ujenzi katika shule ya msingi Mukendo. Shule hiyo ni moja ya wanufaika wa mradi wa majitaka.**



“Maji ni uhai, maji ni maendeleo, maji ni ustaarabu”. Ni moja kati ya maneno yanayotumika kueleza umuhimu wa maji katika maisha ya kila siku, kwa maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla. Uwekezaji katika sekta mbalimbali unahitaji huduma ya uhakika ya maji.

Huduma ya maji ilianza kutolewa tangu enzi za ukoloni katika miaka ya 1930. Ujenzi wa miradi ya maji kwenye vijiji ulianza mwishoni mwa miaka ya 1950 na ilitolewa katika majimbo tisa yaliyokuwepo kwa kipindi hicho ili kukidhi mahitaji ya Serikali ya kikoloni. Huduma kwa wakati huo haikutolewa kwa maelekezo ya kisera.

Hivi sasa Serikali inaendelea kuwekeza katika sekta ya maji ili kuhakikisha wananchi ambao ndio wadau wake wakuu wanaoanza thamani na ubora wa bidhaa wanazozalisha, pia wawekezaji wa viwanda vikubwa na vidogo kuweza kutumia fursa ya uwepo wa huduma ya maji ya uhakika kuwekeza kwa kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali hapa nchini. Ili kuhakikisha maendeleo haya yanawafikia wananchi na hawachukua muda mrefu katika kutafuta huduma za maji, hususan maeneo ya vijijini serikali imeanzisha wakala ya maji ambayo itahusika na huduma ya maji vijijini, kuchimba visima na kusanifu miradi ya maji.

Mwezi Julai, 2019 alama hiyo imewekwa kwa kuanza kazi kwa Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Ni historia iliyoandikwa katika sekta ya maji nchini. Wakala hii moja ya jukumu lake la msingi ni kuhakikisha Watanzania, hususan maeneo ya vijijini wanapata huduma bora ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

RUWASA imeanza kazi kupitia Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira na. 5 ya Mwaka 2019. Sheria hii imeanza kutumika tarehe 1 Julai, 2019. Kutungwa kwa sheria hii ni sehemu ya utekelezaji maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyoyatoa tarehe 10 Mei, 2018. Katika maelekezo yake Mheshimiwa Rais aliagiza, pamoja na mambo mengine, kuwa watumishi wote wa sekta ya maji nchini wasimamiwe na Wizara ya Maji.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiongea katika kikao kazi kilichofanyika Jijini Dodoma hivi karibuni kuhusu uendeshaji wa RUWASA kwa kujumuishwa mameneja walioteuliwa kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini amewataka kufanya kazi kwa bidii na weledi kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi vijijini. Mameneja hao wa RUWASA wametakiwa kuwa mwarobaini wa changamoto za miradi ya maji vijijini, inayoendelea na iliyokamilika kuhakikisha inakua endelevu katika kutoa huduma.

“Tunataka sekta ya maji iwe katika ubora wake muda wote, wananchi wapate huduma ya maji na moja ya kazi tutakazofanya ni kutatua changamoto zilizopo katika miradi ya maji ya vijijini” Naibu Waziri Aweso anasema na kuongeza wataalam wa sekta ya maji waliopewa dhamana wasikubali kusubiri viongozi kwenda vijijini kuona matatizo, bali wao kwa nafasi zao watimize wajibu wao na wasisite kuwasiliana na viongozi wa Wizara ya Maji pale wanapokwama au kutatizwa na jambo lolote wanapotoa huduma kwa wananchi.

Mhe. Aweso anaongeza kuwa miradi yote ya maji itakuwa ikipitiwa na wataalam wa wizara ili kujua thamani yake kabla ya kutekelezwa, na jambo la msingi ni kutoa matokeo kwa wananchi kwa kuhakikisha bomba zinazotoa maji katika maeneo yao.

Katika kikao hicho wataalam wote wa sekta ya maji nchini wametakiwa kushirikiana, kwa wale waliopewa nafasi za uongozi kwa kushirikiana na wale ambao hawakupata. Baadhi ya wataalam hawakupata nafasi kwa sababu ya mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa sekta ya maji, hata hivyo mchango wao unahitajika popote watakapo pangwiwa kufanya kazi.

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo akiongea katika kikao hicho amesema hatua iliyofikiwa ni kubwa na safari ya mabadiliko katika sekta ya maji inaendelea kwa kuweka historia nyingine muhimu. Anasema kwa maendeleo hayo, kila mtu anao uhuru wa

# RUWASA MWAROBAINI WA HUDUMA YA MAJI VIJIJINI



**Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo akiongea katika kikao kazi kuhusu kuanza kazi rasmi kwa RUWASA, jijini Dodoma.**

kutafsiri anavyoweza kwa kufikiwa kwa hatua hiyo, lakini takwimu zinaongea zenyewe na kuweka alama isiyobadilika.

Sekta ya maji katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita imekua na kuleta mabadiliko makubwa katika maisha ya Watanzania. Ni wazi kuwa hakuna jambo la maendeleo linaloweza kufanyika bila uwepo wa maji ya uhakika na mabadiliko yanaonekana kwa uwekezaji na ubunifu uliofanywa na watendaji mbalimbali wa serikali. Miradi ya maji imeongezeka na inaendelea kutekelezwa. Hadi mwezi Aprili 2019 jumla ya miradi ya maji ya kuwahudumia wananchi idadi yake ikiwa 1,659 ilikua imekamilishwa.

Kufikia hatua hiyo, Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Mkumbo anasema kuwa takwimu za hivi karibuni kuhusu huduma ya maji nchini zinaonyesha kuwa kwa mwaka huu 2019 jumla ya idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji ni asilimia 71, ambapo kwa upande wa vijijini ikiwa ni asilimia 65 na mjini ikiwa ni asilimia 84. Hayo ni mabadiliko na hatua kubwa ambapo kwa mwaka 2015 ilikuwa tofauti takwimu zikionyesha wananchi waliokuwa wanapata huduma ya maji wakivi asilimia 56, ambapo kwa maeneo ya vijijini ilikuwa asilimia 46 na mjini asilimia 74.

Prof. Mkumbo anaongeza kuwa sekta ya maji imetoka mbali, na inakoenda ni mbali, na kusisitiza bado matarajio ya wananchi ni makubwa zaidi kuliko hatua iliyofikiwa. Anasema lazima kuongezwa kasi ya utekelezaji wa kazi mbalimbali ikiwamo katika baadhi ya mikoa ambayo bado huduma ya maji ina changamoto.

Anaongeza kuwa kila meneja wa RUWASA atawajibika katika eneo lake kwa kuhakikisha kazi zote zinafanyika kama ilivyopangwa, hivyo ni muhimu kujipanga na kuelewa miradi yote, yenye changamoto mbalimbali na inayoendelea ili kuhakikisha uendelevu wa miradi ya maji vijijini. Prof. Mkumbo anasema malengo ya Serikali ni kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2015, pamoja na miongozo mbalimbali ya kisera imeainisha kuwa nia ni kufikisha huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa kufikia asilimia 95; na miji mikuu ya wilaya, miji Midogo na miradi ya kitaifa kufikia asilimia 90, na vijijini kufika asilimia 85 ifkapo mwaka 2020.

Anasisitiza kwa kueleza kazi iende vizio- viongozi wasaidiwe ukweli, kitalaam ili ri kwa sababu uongo

au kupindisha mambo hakuna nafasi katika kazi.

Prof. Mkumbo anawakumbusha mameneja wa RUWASA kuzingatia Mkataba wa Huduma kwa Wateja katika utendaji kazi kwa kuhakikisha kazi zinafanyika kwa uhakika na sio kwa bahati nasibu. Anasema lazima kuridhika na matokeo na sio kuongea kuhusu mchakato ambao

hauwezi kumsaidia mwananchi anayehitaji huduma ya maji. Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Emmanuel N.M Kalobelo anasema kuwa mameneja wa RUWASA wanatakiwa kutimiza matarajio ya wananchi. “Nye ndio wataalam wa maji na wananchi wanataka kuona bomba zikitoa maji, masuala ya kiufundi ongeeni nye wenyewe, lakini wananchi wanataka matokeo, sio kuweleza mambo mengine” Mhandisi Kalobelo anasema na kusisitiza weledi ukizingatiwa kwa dhati kazi itakuwa nzuri na hakutakuwa na malalamiko kuhusu miradi ya maji. Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA Mhandisi Gonsalves Rutakyamiwa (wakati wa kikao kazi hicho) kuhusu uendeshaji wa wakala hiyo anasema kuwa watahakikisha kazi zinafanyika kwa wakati na huduma kuwafikia wananchi, “Tumejipanga na tutafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kuwa malengo yanafikiwa”.

Mhandisi Rutakyamiwa anasema kuwa kila mmoja katika RUWASA atatekeleza wajibu wake kama inavyotakiwa na suala la kurudishana nyuma halitakuwa na nafasi ili wananchi vijijini wapate majisafi, salama na yenye kutosheleza.

Takwimu zinaonyesha kuwa rasilmali za maji zinazofaa kwa matumizi mbalimbali hapa nchini ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka, kati ya hizo mita za ujazo bilioni 105 zipo juu ya ardhi na chini ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 21. Matumizi yote ya maji kwa sasa yanakadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 40, ambazo ni sawa na asilimia 31.7 ya maji yote yanayofaa kwa matumizi ya binadamu.

Kiwango cha maji kwa mtu ni sawa na mita za ujazo 2,300 (au mapipa 11,500) kwa mwaka. Kiwango hiki ni juu kidogo ya kiwango cha chini cha kimataifa cha mita za ujazo 1,700 kwa mwaka ambapo chini ya hapo nchi huonekana kuwa ina uhaba wa maji. Ni wazi kuwa ongezeko la watu linaendana na mahitaji ya maji kwani mwaka 1962 wastani wa maji kwa mtu kwa mwaka ilikuwa ni mita za ujazo 7,862 (mapipa 39,310).

Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002, inaelekeza wananchi kupata huduma ya maji ndani ya mita 400. Maeneo ya vijijini, huduma ya maji hutolewa kupitia vituo vya maji ambapo kituo kimoja kinasaswa kuhudumia watu wasiozidi 250.

Kazi inaendelea kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya majisafi na salama, mjini na vijijini. Hatua imepigwa, na matarajio bado ni makubwa.

### MAKALA SINGIDA

## Londoni: Kutoka kupiga hodi kuoga wilaya jiradi, Sasa ni ndani ya nyumba

Ni hatua na jambo jipya katika kijiji cha Londoni, hakuna haja ya kutembea kwenda kuoga au kufua mbali na makazi. Huduma ya maji sasa inapatikana kwa wanakijiji. Aidha, nyumba za tembe na miti ambazo uliziacha miaka kadhaa iliyopita, sasa nafasi yake imechukuliwa na nyumba za kisasa za matofali na kuzekwa kwa mabati, tena zikiwa na umeme.

Kupata mahitaji ya msingi kwa binadamu inaweza kuwa safari. Wakazi wa kijiji cha Londoni wilaya ya Manyoni mkoani Singida kutembea kwenda wilaya jirani ya Chemba ili kuweza kuoga na kufua nguo pamoja na mahitaji mengine ya maji ni ratiba iliyozeleka, kwao haikushangaza.

Simulizi za wakazi wa kijiji hicho inasema safari ilikua ikifanyika haswa kipindi cha kiangazi ambapo jua huwa kali, hivyo mhusika anayetaka maji alitakiwa kuamka mapema ili kukwepa hali ya jua kali mchana au kusubiri muda wa jioni. Msimu wa kiangazi maeneo ambayo maji hupatikana wakati wa masika huwa makavu kutokana na maji hayo kuwa ya msimu.

Hata hivyo, safari hiyo iliyokuwa ikichukua wastani wa saa tatu ili kufika katika eneo lenye maji ili kukidhi mahitaji ya wananchi sasa imekua historia kijijini hapo, pia kusadia maeneo ya jirani. Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Maji imewekeza katika miradi mbalimbali ya maji, na moja wapo ni mradi wa maji wa Londoni unaozota huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza kwa wakazi wa eneo hilo.

Serikali kwa kutambua kuwa moja ya eneo la maendeleo kwa wananchi na linaloingizwa kipato ni ufugaji, mradi huo wa maji umeweka mazingira rafiki kwa wafugaji hasa kwa kuweka eneo ambalo mifugo itaweza kupelekwa na kunywa maji. Usanifu huo hauzuii kwa wale watakoenda kuchota maji na kupa mifugo yao ikiwa nyumbani.

Haya yote yanafanyika sio tu kwa kuhakikisha kuwa maji ambayo ni hitaji la msingi kwa kila binadamu linawafikia wananchi mahali walipo, bali kuhakikisha malengo ya nchi katika sekta ya maji ya kufikisha asilimia 85 ya upatikanaji maji vijijini yanafikiwa kama ilivyopangwa ifikapo mwaka 2020.

Mahitaji ya maji kwa matumizi ya nyumbani, ikiwamo biashara na utalii hapa nchini takwimu zinayonesha ni takribani asilimia 46, na umwagiliaji ikiwa asilimia 26, ambayo ndio maeneo yenye mahitaji kwa wananchi wengi wa maeneo ya vijijini.

Kwa nyakati tofauti, wakazi wa Londoni wameongea kuhusu mradi wa maji ulivyobadili maisha yao, kuanzia ratiba za kila siku nyumbani, usafi wa mazingira na afya, hadi hatua nyingine za kujiongeza kipato na ujenzi wa makazi bora zaidi. Wakazi hao wanaonyesha wazi kuwa huduma ya maji imeleta mabadiliko makubwa kama wanavyoshuhudia wenyewe kijijini hapo.

Idi Kisanza mkazi wa kijijini Londoni anasema kuwa kabla ya mradi walikuwa wanapata maji kwa ndoo moja ndogo ya lita 10 tu kwa ajili ya kunywa. Anasema kwa aliye na uwezo kwa wakati huo maji yalipatikana kwa shilingi 2000 kwa ndoo moja kubwa.

"Tulikuwa hatuogi kila siku kwa sababu maji yalikuwa gharama yake" anasema Idi na kuongeza kuwa baada ya mradi wa maji kufika kijijini hapo imekua ahueni kwao na maisha yamekua mazuri kwa sababu ndoo moja inapatikana kwa shilingi 100 tu.

Naye Leah Ezekiel, mama wa nyumbani mwenye familia ya watoto tisa anasema ilibidi kuamka saa nane usiku ili kufuata huduma ya maji, pia kuweza kukamilisha ratiba za kazi nyingine. Anasema pamoja na kuamka saa nane usiku, wingi wa watu, ulisababisha kukaa muda mrefu kupata maji, hadi saa kumi na moja asubuhi ndipo mtu anapata huduma na kuondoka. Anasema kwa familia yake anahitaji madumu 10 kwa siku, hivyo mradi wa maji umekua mkombozi kwake kwa matumizi na kumuwezesha kujishughulisha na kazi nyingine.

Tafti mbalimbali zimeonyesha kwa ujumla kuwa eneo ambalo kuna uhaba wa maji, wanawake hupoteza muda mwingi katika kutafuta huduma hiyo. Hali hii inasababisha kuwakosesha muda wa kutosha kukaa na watoto na kufanya majukumu mengine ya kijamii.

Serikali imewekeza katika sekta ya maji ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo ndani ya mita 400 na hawapotezi muda katika kutafuta maji. Mradi wa maji wa kijiji cha Londoni ni uwekezaji wa serikali kupitia Mfuko wa Maji wa Taifa kwa gharama ya shilingi milioni 382. Mradi huu umewawezesha wananchi



Moja ya nyumba za kisasa kijijini Londoni wilaya ya Manyoni-Singida. Kushoto ni nyumba ya tembe na miti. Mradi wa maji wa uliofanikishwa kijijini hapo na serikali umeleta mabadiliko makubwa katika maisha ya wananchi ikiwamo kuboresha makazi kwa kujenga nyumba za kisasa.

kutumia shilingi 100 badala ya shilingi 2000 waliyokuwa wakutumia awali kununua dumu moja la maji, ambalo hawaku na uhakika na usalama wake.

Mwanahamisi Kisanza anasema kuwa huduma ya maji kabla ya mradi huo ilikuwa sio ya uhakika na uwezo ulikua wa kupata madumu mawili tu kwa siku, kwa maana ya shilingi 4000. Hivyo, ili kuhakikisha maji yanatumika kwa utaratibu ilibidi kuyagawa katika lita tano tano, ambapo watoto wake aliwaogesa kwa mbinu ya kuwaloweka bila kumwaga maji chini, hivyo kuogesa watoto kwa mkupua na kutumia maji kiasi kidogo kuondoa sabuni. Kisanza anasema hiyo ndivyo hali halisi iliyokuwa kutokana na gharama za kununua maji.

Anaongeza kuwa katika mahitaji ya nyumbani, haikua rahisi kununua vyakula vinavyotumia maji mengi katika maandalizi kwa sababu vinaongeza gharama ya matumizi. Kisanza anafafanua kuwa hata kushiriki kazi za kijamii kama mikutano baadhi ya watu hawakupenda kutoka na ukweli kuwa walikuwa wanaogopa kutokana na maandalizi kuhitaji maji yakutosh.

Kisanza anasema ujio wa mradi wa maji wa Londoni umeleta mabadiliko makubwa kuanzia maisha ya nyumbani, usafi wa mazingira, afya na makazi. Anasema maisha yamebadilika kwa kiwango kikubwa, na maendeleo yanaonekana kwa wakazi wa Londoni kwa kutoka katika makazi ya nyumba za Tembe na Miti hadi nyumba za kisasa za matofali ya kuchoma, zikiwa na huduma ya umeme.

Mganga Mfawidhi Dkt. Dimoso Mbezi anayefanya kazi katika Zahanati ya Londoni anasema huduma ya maji imewasaidia katika kazi kwa kiwango kikubwa, kwa kutosa huduma bora zaidi. Anasema maji ni hitaji la uhakika kwa kina mama wakati wa kujifunga, pia kuepusha magonjwa yanayosababishwa na maji, hivyo kupunguza gharama zinazotumika kukabiliwa na magonjwa yanayoendana na matumizi ya maji yasiyo salama. Hivyo, Dkt. Mbezi anasema mradi wa maji umekua moja ya mafanikio makubwa katika sekta ya afya kijijini hapo.

Asha Mohammed, aliyejaliwa kujifunga watoto wawili katika Zahanati ya Londoni anasema awali kabla ya mradi wa maji wakati wa kujifunga ilikuwa kazi zaidi, ilihitaji kufanya maandalizi mapema, kwa kununua maji ya kutosha nyumbani kwa matumizi baada ya kutoka hospitali. Anaongeza kwa asiyeweza kununua maji ilimlazimu kutembea umbali mrefu kufika katika Bwawa la Mpondi, mpakani mwa Wilaya ya Chemba kuchukua maji. Naye Amina Hussein, mama wa watoto wawili anafafanua kuwa baada ya mradi wa maji kufika kijijini mahitaji ya maji kwa mama anayejifunga imekua rahisi na kuwa nadhifu zaidi.

Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi Londoni Bw. Claudi Kamate anasema mahudhuria ya yamekua bora zaidi

baada ya shule kuwekwa bomba. Anasema hata hali ya usafi wa wanafunzi shuleni imekua nzuri tofauti na awali, ambapo shule imeweza kuotesha miti na kuboresha mazingira ya wanafunzi kusoma.

Janet Innocent, mwanafunzi katika shule hiyo anadhihirisha hilo kwa kusema kuwa hivi sasa wamekua nadhifu zaidi, na mazingira yamekua bora kwa kuwa na maua ya kutosha katika bustani zinazozunguka shule yao.

Mwalimu Mkuu Msaidizi, Shule ya Msingi Londoni Bi. Veronika Mawanza anasema shule hiyo yenye wanafunzi 1153 inapata madumu 60 kila siku bila malipo, ambapo matumizi ya wanafunzi kwa maji ya kunywa ni wastani wa pipa kwa siku. Mwalimu Veronika anasema maji yamewawezesha kujiongeza mambo ya ziada ambayo hayakuepo, mfano hivi sasa wanalima bustani na kujipatia mboga mboga za kutosha.

Meneja wa Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) wilaya ya Manyoni Eng. Gabriel Ngonzi anasema huduma ya maji kwa wananchi katika mradi wa Londoni inapatikana kwa kutumia mtambo wa kusukuma maji unaozumia nishati ya mafuta, kwa bei ya shilingi 100. Hata hivyo, baada ya umeme kufika kijijini hapo gharama hizo zitashuka zaidi na kuwawezesha wananchi kuongeza thamani ya bidhaa wanazozalisha.

Hivyo, wananchi wote mjini na vijijini wanapaswa kuelewa uchumi wa viwanda unahitaji usimamizi bora wa rasilimali za maji. Umeme wa kutosha kukidhi mahitaji ya viwanda na majumbani unategema uwepo wa maji ya kutosha. Kazi ya kulinda na kuendeleza vyanzo vya maji ni jukumu la kila mwananchi.

Hakika huduma za maji katika maeneo ya vijijini itazidi kuimarika. Kama inavyoelweka Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) imeanza kazi mwezi Julai, 2019. RUWASA ni ufupisho wa Rural Water Supply and Sanitation Agency. Ni Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019.

Wakala hii, pamoja na kazi nyingine ina majukumu ya; Kusanifu na kusimamia ujenzi wa miradi ya maji vijijini, kufanya utafti kuhusu maji chini ya ardhini, Kuchimba visima na kujenga mabwawa, Kusajili na kuviwezesha vyombo vya watumiaji maji vijijini, Kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika maendeleo ya sekta ya maji vijijini na Kumshauri Waziri wa Maji kuhusu uendeshaji wa sekta ya maji vijijini.

Kupitia RUWASA huduma za maji vijijini zitazidi kuimarika na kuleta mabadiliko na maendeleo zaidi katika maisha ya kila siku kwa wananchi. Mradi wa maji wa Londoni una vituo 12 vya kuchotea maji vinavyofanya kazi na eneo maalum la mifugo kunywa maji.



# RUHILA WALIPWA FIDIA

**S**erikali imelipa kiasi cha shilingi 1,913,832,491/= ikiwa ni fidia kwa wananchi waliokuwa na makazi kando kando ya bonde la mto Ruhila ambalo ni chanzo cha maji cha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA).


Wananchi hao wamekuwa wakifuatilia malipo yao kwa miaka 15 iliyopita tangu mwaka 2003. Malipo hayo yamefanyika kwa awamu tatu (3); awamu ya kwanza kiasi kilicholipwa ni Shilingi 500,000,000/= na awamu ya pili na ya tatu kiasi kilicholipwa ni Shilingi 1,413,832,491.

Zoezi la kuwalipa wananchi hundi zao limesimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA).

Idadi ya wananchi waliolipwa fidia ni 723. Hata hivyo, idadi ya wananchi wapatao 80 hawakujitokeza kuchukua hundi zao ambazo bado zipo katika Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA), wananchi wanatakiwa kufika katika ofisi hizo ili wakabidhiwe hundi zao.



Miongoni mwa wananchi baada ya kukabidhiwa hundi zao





# RUWASA YAPELEKA MAJI VIJIJINI

**M**tambo (Rig. Na. 84) wa RUWASA ukiongozwa na Rig. Incharge Elia Samweli ukiwa eneo

la tukio katika kijiji cha Nyang'olo mkoani Iringa. Mtambo huu unatekeleza mradi wa kuchimba visima viwili viwili (2)

kutoka kwa mteja ASAS Ltd ambapo kisima cha kwanza kimepata maji lita za ujazo 50,000 kwa saa.

## RUWASA YAPATA MKURUGENZI MKUU

Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb), kwa kuzingatia mamlaka aliionayo kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019, amemteua Eng. Clement Lenard Kivegalo kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (Rural Water Supply and Sanitation Agency-RUWASA) kuanzia tarehe 01 Agosti 2019.

Taarifa ya Kaitibu Mkuu, Wizarara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo ya Agosti 5, 2019 inasema Eng. Clement Kivegalo ana Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Uhandisi wa Rasilimali za Maji (MSc Water Resources Engineering) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na amesajiliwa na Bodi ya Usajili ya Wahandisi Tanzania (ERB). Aidha, Eng. Kivegalo ana uzoefu wa miaka 18 katika Sekta ya Maji, kati ya hiyo miaka 12 ikiwa katika nafasi mbalimbali za uongozi katika Sekta ya Maji. Wasifu wa Eng.

Kivegalo ni pamoja na kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa kwanza wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Kahama-Shinyanga (KASHWASA). Mamlaka hii ndiyo iliyosimamia mradi mkubwa wa kwanza wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenenda katika Miji ya Kahama na Shinyanga.

### Kuhusu RUWASA

RUWASA ni ufupisho wa Rural Water Supply and Sanitation Agency, ikiwa ni Wakala ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Wakala hii ina jukumu la kusimamia ujenzi wa miradi ya maji vijijini, na

kuhakikisha kuwa huduma ya maji vijijini inawafikia wananchi walio wengi kwa mujibu wa malengo ya kitaifa.

Tunachukua nafasi hii kumtakia Eng. Clement Lenard Kivegalo mafanikio katika utekelezaji wa majukumu makubwa ya kuiongoza Taasisi mpya ya RUWASA na katika kuhakikisha kuwa huduma ya maji vijijini inaimarika.

**Tunachukua nafasi hii kumtakia Eng. Clement Lenard Kivegalo mafanikio katika utekelezaji wa majukumu makubwa ya kuiongoza Taasisi mpya ya RUWASA na katika kuhakikisha kuwa huduma ya maji vijijini inaimarika.**





# MAJI BILA FOLENI YAWAINUA NAMANGALE

**M**iaka ya hivi karibuni sekta ya maji imekuwa ikiimarika kutokana na upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa maeneo ya vijijini. Huduma hii imeshuhudiwa ikipatikana kwa gharama nafuu zaidi na hivyo wananchi wa maeneo hayo kukiri hatua kwa hatua wame-timiza lengo.

Hayo yanaelezwa na wakazi wa baadhi ya maeneo ya vijijini, hususani maeneo ya vijiji vya Utimbu-la, Namangale A na Namangale B vya Halmashauri ya Lindi vijijini ambavyo vinapata huduma ya majisafi ya bomba kwa gharama nafuu wanayoimudu.

Wakazi hao zaidi ya 5,000 wanapata huduma ya majisafi kwa shilingi 1,000 kwa mwezi kwa kila kaya kwa wananchi wanaocho-ta maji kwenye vituo vya kuchotea maji vya jamii bila kujali kiasi cha maji watakayochota, na shilingi 2,500 kwa kila kaya kwa mwezi kwa wananchi ambao wameunganishiwa maji katika makazi. Gharama hizi ni nafuu ukichukua uhalisia wa gharama za uendeshaji wa mradi, uzalishaji wa maji na nishati.

Imezeleka kuwa, katika baadhi ya maeneo wananchi wamekua wakinunua maji kwa gharama ambayo ni kubwa kidogo ukilinganisha na mkoani Lindi.

Hawa Makwita ni Mtendaji kata wa Namangale anaeleza namna wanaoendesha mradi wa maji wa Namangale.

“Huduma ya maji kwa vijiji vyote hutolewa kwa gharama ya shilingi elfu moja kwa kila kaya kwa mwezi, na shilingi 2500 kwa mwezi mmoja kwa kaya zitakazovuta maji nyumbani na gharama ya kuunganisha maji kwa kaya

ni shilingi 30,000 tu” Hawa anasema. Anaongeza kuwa katika mradi huu, kuna vituo 16 katika maeneo mbali mbali kwa vijiji vyote vitatu ambavyo husaidia wananchi kupata huduma ya maji kwa haraka na bila foleni.

Mradi wa maji wa Namangale ulianza kutekelezwa mwaka 2013 na kukamilika mwaka 2017 ambapo jumla ya wakazi 5,000 wanapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza karibu na makazi yao. Kabla ya kukamilika kwa mradi huu, wakazi wa maeneo hayo walikuwa wakichota maji kwenye makorongo kwa wastani wa kilometa tano au zaidi, ambapo walikuwa wakitumia muda mwingi kufuata maji maeneo ya mbali ambayo hawakua na uhakika wa ubora wake.

Wakazi hawa walikuwa wakikumbana na changamoto mbali mbali, zikiwemo wanyama, kupoteza muda mwingi wa kufuata maji na hivyo kuathiri shughuli zao nyingine za kiu-chumi, pia magonjwa yanayotokana na matumizi ya maji yasiyo salama.

“Mradi huu umekuwa ni mkombozi sana kwa maeneo yetu haya, kwani sasa wananchi wa maeneo haya wanafanya shughuli zao za kiuchumi haswa kilimo cha ufuta na kujiongeza kipato. Kabla ya huu mradi hata nyumba za wananchi zilikuwa hazina ubora huu unaouona sasa” Masoud Kanduru diwani wa kata ya Namangale anasema.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafanya jitihada mbalimbali ili kuwakomboa na kuwa-ondolea adha wananchi wa Tanzania waishio mijini na vijijini kwa kuwapatia huduma ya majisafi na salama karibu na makazi yao.

Kwa mujibu wa Sera ya Maji ya mwaka 2002, maji

yanayosambazwa kwa matumizi ya binadamu lazima yawafikie wananchi husika katika umbali usiozidi mita mia nne (400) na vilevile huduma hii isimamiwe kwa ustadi na ufanisi katika ujenzi, uendeshaji, utunzaji na uhifadhi wa vyanzo na miundombinu ya maji iweze kuwa endelevu na kuwafikia wananchi wengi zaidi. Kutokana na maagizo yaliyomo kwenye Sera na kwa kutambua kuwa maji ni rasilimali adimu na muhimu katika maisha ya binadamu, Serikali imekuwa ikiandaa mikakati ya kuifanya rasilimali hii kuwa endelevu na kutosheleza mahitaji.

Katika ahadi yake kwa Watanzania wakati aki-omba ridhaa ya kuiongoza Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kutumia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) azma kuu ilikua kufikisha majisafi na salama kwa wakazi wa vijijini kwa asilimia 85 na mijini kwa asilimia 95 na kwa makao makuu ya wilaya kwa asilimia 90 ifikapo 2020.

Hadi kufikia mwezi Juni, 2019 jumla ya miradi 44 ya vijijini ilitekelezwa na kukamilika mkoani Lindi ambapo ilichangia jumla ya vyombo 153 vya watumiaji Maji kusajiliwa katika katika Halmashauri zote za Mkoa wa Lindi. Kukamilika kwa miradi hii kumepolekea hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kungezeka hadi kufika asilimia 56 ya wakazi waishio vijijini.

Utekelezaji wa mradi wa maji wa Namangale ni kielelezo cha mafaniko waji tokanayo na uanzishwaji wa Mfuko wa Maji wa Taifa (National Water Investment Fund –NWF) ambapo tangu kuanzishwa kwake katika kipindi cha zaidi ya miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016

hadhi kufikia mwaka 2018/2019 jumla ya Shilingi 540,615,053,320.91 sawa na asilimia 95 ya makadirio ya makusanyo ya muda wote wakipindi cha miaka minne, zilikusanywa na kupelekwa kwenye miradi ya maji kwa kipindi hicho cha takriban miaka minne. Hivyo, miradi mingi ya sekta ya maji sasa hukamilika kwa wakati na kuwa-ondolea wananchi adha ya kupata huduma ya majisafi na salama.

Mfuko wa Maji wa Taifa (NWF) umeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 44 cha Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira. Pamoja na kuanzishwa kisheria mwaka 2009, utekelezaji rasmi wa majukumu ya Mfuko ulianza mwezi Machi, 2015 baada ya kupata chanzo cha mapato cha uhakika kutoka katika tozo ya mafuta pamoja na kuundwa kwa Sekretarieti ya Mpito. Majukumu ya Mfuko wa Maji wa Taifa ni kutafuta rasilimali fedha, kutoa fedha hizo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na kufuatilia matumizi ya fedha hizo. Lengo kuu la Mfuko ni kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji na usimamizi wa maeneo ya vyanzo na vidakio vya maji, kipaumbele kikiwa kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa huduma ya maji hususan vijijini. Pia, miongoni mwa kazi za Mfuko ni kusaidia uwekezaji katika ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji vijijini, kutoa fedha kwa ajili ya upanuzi wa miradi ya maji mijini hususan kwenye makao makuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa, pamoja na kuwekeza kwenye usimamizi na uendelezaji wa vyanzo vya maji ili kuboresha upatikanaji wa huduma na endelevu wa rasilimali za maji nchini.



Waziri wa Maji Mhe. Profesa Makame Mbarawa akiangalia ubora wa kizimba na bomba zilizotumika katika kizimba cha kupunguza msukumo wa maji (BTP) katika eneo la mashamba la Simba. BTP moja ya kazi yake ni kuzuia mabomba kupasuka. Mradi wa maji wa Longido bomba kuu limelazwa kwa umbali wa kilomita 94. Thamani ya mradi ni kiasi cha Shilingi bilioni 15.7.



Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Maji wa Taifa Mhandisi Abdallah Mkufunzi, akitoa neno la kuaga katika siku yake ya mwisho baada ya miaka 42 kama mtumishi wa umma kwa menejimenti ya Wizara ya Maji jijini Dodoma. Mhandisi Mkufunzi amestaafu kazi, tunampongeza na kumtakia kila kheri.





## SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA, NAMBA 5 YA MWAKA 2019

Sheria hii imeanza kutumika tarehe 1 Julai, 2019. Pamoja na mambo mengine, Sheria imeainisha masuala ambayo hayaruhusiwi. Masuala hayo ni kama ifuatavyo;

### MAKOSA YA JINAI NA ADHABU

#### # NI KOSA

KUHARIBU MIUNDOBINU YA MAJI SAFI NA MAJITAKA AU MALI.  
ADHABU YAKE INAANZIA FAINI YA SHILINGI LAKI TANO HADI MILIONI TANO AU KIFUNGO KISICHOPUNGUA MIAKA MIWILI HADI MIAKA MITANO, KWA MUJIBU WA KIFUNGU CHA 61

#### # NI KOSA

KUCHUKUA MAJI AU KUCHEPUSHA MAJI KUTOKA KWENYE MIUNDOBINU YA MAJI  
ADHABU YAKE INAANZIA FAINI YA SHILINGI LAKI TANO HADI MILIONI TANO AU KIFUNGO KISICHOPUNGUA MIEZI 12 HADI MIAKA MITANO NA KULI-PA GHARAMA ZA UHARIBIFU, KWA MUJIBU WA KIFUNGU CHA 62

#### # NI KOSA

### KUTUMIA MAJI VIBAYA (MISUSE OR WASTE)

ADHABU YAKE INAANZIA FAINI YA SHILINGI LAKI TANO HADI SHILINGI MILIONI KUMI, AU KIFUNGO KISICHOPUNGUA MIEZI SITA HADI MIAKA MIWILI, KWA MUJIBU WA KIFUNGU CHA 63

*Itaendelea...*



Naibu Waziri wa Maji Mhe. Juma Aweso (Mb) akiwa katika kikao kazi na madereva wa Wizara, katika mji wa Serikali Mtumba, jijini Dododoma



Mwaka mmoja wa mafanikio DAWASA



# Ni mwaka mmoja wa mafanikio DAWASA

- Ni baada ya kuunganisha shughuli za DAWASA na DAWASCO
- Miradi 15 yatekelezwa katika maeneo ambayo hayakuwa na maji
- Wananchi lukuki waunganishiwa huduma ya Maji.



Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA Jenerali Mstaafu Davis Mwamunyanje akiwa na baadhi ya Wajumbe wa Bodi walipotembelea mradi wa Maji katika Mji wa Mkuranga unaosimamiwa na DAWASA na kuona shughuli za ulazaji wa mabomba na ujenzi wa tanki la Maji lenye ujazo wa lita Milioni 1.5.

## Mwandishi wetu, Mwananchi

Tunaweza kusema ni Mwaka mmoja wa mafanikio kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (DAWASA) tangu kuunganishwa kwa DAWASA kwa DAWASCO. Aidha Menejimenti ya Mamlaka hii ilizinduliwa rasmi Septemba 8, 2018. Ilikuwa ni jambo la busara kuunganisha taasisi hizi mbili ili kuunda Mamlaka kubwa na yenye nguvu miongoni mwa Mamlaka za Maji nchini.

### Nini siri ya mafanikio haya kwa muda mfupi?

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa DAWASA, Mkuu wa Majeshi Mstaafu Jenerali Davis Mwamunyanje anabainisha kuwa siri ya mafanikio yaliyopatikana ndani ya kipindi hiki kifupi ni uongozi IMARA uliokuwa na malengo ya kufikisha huduma kwa wananchi wengi zaidi pamoja na utayari wa watumishi wa Mamlaka katika kutoa huduma bora ya Majisafi na Majitaka. “Katika yote tunajivunia



Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb) akisoma mita ya mteja eneo la Sinza jijini Dar es Salaam wakati wa zoezi la usomaji na uhakika na Mita za Maji za wateja wa DAWASA lililofanyika hivi karibuni.

utayari wa watumishi wetu katika kuandaa mipango endelevu na kutekeleza kwa vitendo maagizo ya viongozi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya majisafi na

majitaka,” alisema Jenerali Mstaafu Mwamunyanje.

Mwaka mmoja wa DAWASA mpya kwangu mimi kama Mwenyekiti wa Bodi na wajumbe ndani ya Bodi

ninayoiongoza inatupa faraja ya kuona Mamlaka tunayoisimamia inafanya kazi nzuri inayoonekana na wananchi wawahudumu.

Katika kipindi cha mwaka mmoja, miradi mingi iliyoleta ahueni kubwa kwa wananchi ndani ya eneo la huduma la DAWASA imetekelezwa. Miradi ipatayo 15 imekwisha kamilika nayo ni pamoja na Mradi wa Maji Tabata Bonyokwa, Tabata Kisukuru, Mradi wa Maji Kiwalani awamu ya pili na ya tatu, Mradi wa Maji Saranga, Kiembeni, Kito-peni, Kilimahewa, Lulanzi, Salasala, Zinga na Mradi wa Maji Zinga Moto. Hivi sasa wananchi katika maeneo hayo wanaendelea kupata huduma.

Vilevile alianisha Miradi kumi ya maji inayotarajiwa kuanza kutekelezwa hivi karibuni ambayo ni pamoja na Mradi wa Maji Minazi minane, Makurunge awamu ya pili, Mingo awamu ya pili, Mabwepande, Kilindoni, Kidunda, Zegereni, Disuny-ala, Kibaha Tamco/ Pangani na kazi ya kuweka mtandao wa Maji eneo la Buza.

“Tulipoanza usimamizi

wa Bodi hii, Mamlaka ilitenga asilimia 30 ya mapato yake katika utekelezaji wa miradi. Sasa imeongeza kiwango na kutenga asilimia 45 ya mapato yake katika usimamizi na utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya majisafi na majitaka itakayoweza kufikisha lengo la asilimia 95 ya upatikanaji majisafi na 30% ya huduma ya majitaka ifikapo 2020,” alimalizia Jenerali Mstaafu Mwamunyanje.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja anasema hadi sasa Mamlaka imefanikiwa kusambaza maji safi na salama kwa asilimia 85 jijini Dar es Salaam.

“Zawadi yetu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. John Magufuli hadi kufikia Disemba 9 mwaka huu ni kukamilika mradi wa Maji wa Chalinze- Mboga utakaohudumia wananchi takribani 125,000,” anasema Mhandisi Luhemeja, na kuongeza kuwa katika kipindi hicho ana hakika kuwa mradi wa Kisarawe nao utakuwa umekamilika. Mradi wa Kisarawe ni agizo la Mheshimiwa Rais wakati akizindua mtambo wa Ruvu Juu, Juni 21, 2016.

Mhandisi Luhemeja anabainisha kuwa awali mwaka 2015 Jiji la Dar es Salaam lilikuwa linapata maji kwa asilimia 68 na jumla ya maunganisho ilikuwa 123,000.

“Kwa wakati huo upotevu wa maji ulikuwa asilimia 53 na Shirika la DAWASCO ilikuwa inakusanya kiasi cha Tsh Bil 3.2 kwa mwezi. Leo hii tunapongea hali ya upatikanaji maji Jijini imepanda hadi asilimia 85 na maunganisho ya maji yameongezeka kutoka 123,000 hadi kufika 326,000. Aidha upotevu wa Maji kwa mwezi Agosti tunapomalizia mwaka mmoja tunaweza rekodi ya kufikia asilimia 39 ya kiwango cha Maji yasiyolipwa,” anasema Luhemeja. Ameahidi kuwa jitihada hazitaishia hopo hadi pale ambapo huduma zinazotolewa na DAWASA zitakapokuwa kiwango cha kima-





### Mwaka mmoja wa mafanikio DAWASA



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo akikagua ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo wa lita milioni 6 litakalohudumia Wilaya ya Kisarawe pamoja na maeneo Pugu, Chanika, Majohe na Gongo la Mboti.



Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA Jenerali Mstaafu Davis Mwanunyangi akisikiliza maelezo kutoka kwa baadhi ya wajumbe wa bodi hiyo, walipotembelea mradi wa Maji katika Mji wa Mkuranga unaosimamiwa na DAWASA na kuona shughuli za ulazaji wa mabomba na ujenzi wa tanki la Maji lenye ujazo wa lita Milioni 1.5.



Waziri wa Maji Mhe. Prof Makame Mbarawa akisoma mita ya maji katika kiwanda cha saruji Twiga kilichopo eneo la Wazo jijini Dar es Salaam.

mkopo kwa yeyote anayehitaji kuunganishwa huduma," alisema na kuwataka wananchi kutoa ripoti kwa vyombo vya dola kwa yeyote atakayekuwa anatoza fedha kwa ajili ya maunganisho.

Katika kuendeleza azma yake ya kuboresha huduma, DAWASA inaendelea kutekeleza Jumla ya miradi 23 ya Majisafi katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya miji ya Mkoa wa Pwani. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi

#### UTEKELEZAJI WA MIRADI MIKUBWA YA MAJI

Julai mwaka huu DAWASA walitia saini utekelezaji wa miradi sita mikubwa ya Usambazaji maji katika miji Dar es Salaam na maeneo ya miji ya Pwani.

- Mradi wa Usambazaji Maji kuanza Matanki ya Chuo Kikuu hadi Bagamoyo.
- Mradi wa Bomba la kusafirisha Maji kutoka Jet hadi Buza.
- Mradi wa Kuchimba Visima ishirini (20) Kimbiji na Mpera.
- Mradi wa Usambazaji Maji Kisarawe- Pugu (Gongo la Mboti, Pugu station, Airwing, Ukonga na Majohe)
- Mradi wa Maji katika Mji wa Mkuranga.
- Mradi wa bomba la kusafirisha Maji kutoka Mlandizi (Ruvu Juu) hadi Kijiji cha Mboga (Chalinze).

kulipia huduma," alisema na kuingeza kuwa wateja pia wamekuwa wakikumbushwa mara kwa mara njia za malipo ili kuweza kulipa kwa wakati huduma muhimu ya Maji.

Akishukuru wateja wote kwa uaminifu waliouonyesha kwa Mamlaka katika kipindi cha mwaka mmoja Afisa Mtendaji Mkuu alihadi kuboresha utendaji wa Mamlaka kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili huduma iendelee kupunguza gharama za uendeshaji. "Nichukue fursa hii kusema katika kipindi ambacho serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani DAWASA haijapandisha bili ya maji pia niseme DAWASA haina mpango wa kupandisha bili za maji katika kipindi chote cha uongozi wa serikali ya awamu ya tano," anasema Mhandisi Luhemeja.

Mhandisi Luhemeja anasema DAWASA inaendelea na mpango wake wa kuunganisha wateja kwa mkopo ambapo wengi sasa wanajitokeza.

"Nitumie fursa hii kuwajulisha wananchi kwamba maunganisho ya huduma za maji ya DAWASA ni kwa

wa Maji Kibamba- Kisarawe, Jet- Buza, Kisarawe- Pugu, Mradi wa Maji Maneromango, Mradi wa Maji Mkuranga, Mradi wa Maji Gezau- lolo, Tungutung, Kiharaka, Mpji, Stakishari, Majumba sita, Vingunguti, Kipawa, Sanzale, Ukuni, Ujenzi wa tanki la kuhifadhi Maji mji wa Bagamoyo, Mradi wa Maji Nyakasangwe, Mradi wa Maji Nia njema na Mradi wa ulzaji wa bomba kubwa la Majisafi kutoka Mlandizi hadi Maneromango.

Kwa mujibu wa Mhandisi Luhemeja, miradi mingine mipya 10 inatarajiwa kutekelezwa na lengo ni kwenda kujibu kero za wakazi hao wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani.

Utekelezaji wa Miradi hii ni ishara na dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dk John Magufuli kuwaondolea wananchi changamoto ya upatikanaji wa huduma ya Majisafi jijini Dar es Salaam na mkoani Pwani.



## MOSHI URBAN WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY



### Tumia Control Namba

yako sasa kulipia Bili yako ya Maji

Lipia Kwenye Tawi la Benki au kwa Wakala  
yoyote wa Benki ya CRDB na NMB  
aliye Karibu Nawe.

Kwa Kutumia Control Namba yako  
inayoanza na namba 99163  
utakayopewa kila Mwezi Na Mamlaka Ya Maji  
Moshi MUWSA.

 [twitter.com/MajiMoshi](https://twitter.com/MajiMoshi)

 [@muwsa\\_moshi](https://www.instagram.com/muwsa_moshi)

© muwsa 2019



## KM MAJI PROF. KITILA MKUMBO ANASEMAJE?

JULAI - OKTOBA, 2019

“RUWASA inakuja na sura mbili ambazo ni kutatua changamoto za kimfumo na kiutendaji. The beginning will be tough but the future of RUWASA is very bright. Put your house in order quickly; that's highly important and a matter of urgency”

“Civil servants must internalize the ruling party manifesto that has made up the government, but need to be impartial and objective”

“A manager, in principle has to manage an average of ten people”

“Communication Officers in the Water Sector, need to be informed, brand the image of the Ministry and report carefully. Make the Ministry positively visible”



**Prof. Kitila Mkumbo**  
Katibu Mkuu - Wizara ya Maji

“Kazi mliyo tutuma ya kuanzisha RUWASA tumeimaliza, sasa ninyi Wataalam mtimize wajibu wenu. Tujipange kujibu malalamiko na kutatua changamoto, kila mmoja achukue nafasi yake ili tusikwazane bali tubebane. Tulenge matokeo, sio michakato”

“Kazi ya kusambaza maji inaendelea kwa kasi kubwa sana nchini. Katika Kanda ya Ziwa peke yake kuna miradi 18 yenye thamani ya jumla ya shilingi Trilioni 1.3 ambayo itakamilika kwa wakati na itoboresha hali ya maisha ya wananchi”

“Changamoto ya DDCA ni hand to mouth. Jitahidini mjiendeshe kibiashara; mjitegemee. Ninyi sio service provider. Establish your average capacity ya kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa kwa mwaka na muweke mpango kazi wa kuzunguka mkitekeleza kazi hizo. Hii itasaidia Wilaya fulani kujua itafikiwa lini”

“**Wataalam mtusaidie sisi viongozi kwa kutuambia ukweli na kutushauri kitaalam. Uongo ni sumu katika professionalism**”

